LEARNING BY EAR EPISODE – Girls
8th EPISODE: Personal Hygiene.
Text: Zainab Aziz
Redaktion: Andrea Schmidt/Christine Harjes

CHARACTERS.........
Anchor: Intro / Autro
BIBIY.....Main Character
Rossie.......same character
Alma.........same character
Cultural officer..........Male Adult.
Teacher...........Woman Adult.

Intro:
Hujambo na karibu kwenye sehemu ya nane ya mfululizo wa makala ya Jifunze Kwa Kusikiliza.Makala haya yanaangazia maswala mablimbali yanayowakabili wasichana. Leo hii Bibiy na wenzake wanaangazia swala la usafi na umuhimu wake kwa wasichana hasa katika siku za mwezi ambazo zinawasumbua wasichana wengi. Je Bibiy na wenzake wanapanga kufanya nini?

Sign Tune....

SCENE ONE:
TEACHER: Wasichana leo hii nataka tuzungumzie swala muhimu, kama mtakumbuka Bibiy alileta pendekezo kuwa tuanzishe kampeni ya kuwahamasisha wasichana kuhusu usafi na hasa wakati wa siku za mwezi,nimfikiria sana juu ya wazo hili naona kuwa lina umuhimu tulizungumzie zaidi..Enhee. hebu Bibiy tuelezee zaidi.

BIBIY: Ndio mwalimu, kwa sababu mara nyingi hutokea kuwa wasichana wengi hushindwa kabisa kuzungumzia swala la siku za mwezi waziwazi hata na wazazi wao..kwa hiyo inakuwa vigumu sana kwa wengi wetu kuweza kujua ni kipi hasa tunachohitajika kufanya ili kulinda usafi na afya zetu..kwa mfano kuna baadhi ya wasichana wanaa amini kuwa ukiwa katika siku zako za mwezi basi hupaswi hata kuoga au hupaswi kwa mfano

kufanya mazoezi ya viungoau kukimbia na hiyo si kweli kabisa...kwa hiyo mwalimu kampeni ambayo nimependekeza tuifanye ni kuhusu kupambana na mawazo potofu kama hayo na pia kuweza kuwasaidia wasichana wenzetu wafahamu mengi kuhusu hali hiyo.

TEACHER: Asante sana Bibiy pendekzo hilo ni la muhimu na sote tunafaa kulititilia maanani..kuhusu kutokuzingatia usafi hasa wakati wa siku za mwezi mara nyingi kunatokana na kuwa na mawazo potofu katika jamii lakini ukweli ni kwamba lazima wasichna wazingatie hali ya usafi wa hali ya juu wakati huo. Naam Rossie na wewe una mawazo gani?
ROSSIE: Mimi naongezea tu kwa kusema, kuwa usafi una maanisha mtu kujijali zaidi katika usafi wake binafsi kwani kwa kufanya hivyo kunamuongezea msichana utulivu na pia kujiamini nafikiri labda wasichana wengi huwa wnaona aibu kuuliza maswali kuhusu hedhi.

TEACHER: Ndio maana katika kampeni ambayo mmeipendekeza ningependa mtilie mkazo swala la kujiamini..kwa kuwa ikiwa hujiamni huwezi kufanya lolote kwani kila mara utakuwa umegubikwa na woga na wasiwasi. na sasa tukianza na nyinyi wenyewe hapa darasani nani anaweza kutueleza kuhusu yeye mwenyewe.enhe naona pale mikono mingi imeinuliwa.. haya Alma hebu tuelezee.

ALMA: Mimi nilianza kupata siku zangu za mwezi nilipokuwa miaka 13, kwanza nilikuwa natumia kitambaa ambacho ilinibidi nikifue halafu kukiweka ili kuweza kukitumia tena wakati mwingine, nilifundishwa na bibi yangu kutumia kitambaa lakini kwa kweli nilikuwa nasumbuka sana hasa kuhusu kuzingatia usafi,yaani usafi wangu mimi mwenyewe binafsi na pia kukiweka kitambaa changu katika hali safi yaani kukifua mpaka kitakate hiyo ilikuwa taabu sana kwangu. pili mara kwa mara niliaibika shuleni kwa kuwa nguo zangu ziliharibika, kwa sababu kitambaa kile hakikuweza kunihifadhi vyema.

TEACHER: Anhaa! Na wakati ulipokuwa unatumia kitambaa

mara ngapi ulikuwa unabadilisha?

ALMA: Wakati mwingine nilikaa na kile kitambaa hadi kwa muda wa saa kumi na mbili au saa kumi na tatu hivi, nashukuru shangazi yangu akanizungumzia juu ya madhara ya kutokuzingatia usafi wakati wa hedhi, baadae nikaanza kutumia taulo maalum ambazo nilibadili kila baada ya saa tatu au saa nne hivi, mapaka sasa natumia taulo hizo maalum.

BIBIY: Mwalimu mimi nafikiria pia jambo lingine linalochangia hali ya kutozingatia usafi wakati wa hedhi ni kwamba wazazi wengine hawawapi watoto wao fedha za kununulia taulo maalum kwa hivyo wasichana wanalazimika kuendelea kutumia njia za kienyeji ili kujihifadhi wakati wa siku zao za mwezi.

TEACHER: Vizuri sana wasichana maelezo yenu yanaonyesha wazi kuwa mna ukakamavu wa kutosha yaani mmeweza kujieleza vizuri kabisa..nimevutiwa sana na uwezo wenu mkubwa, nakubaliana nanyi kuwa wasichana lazima waulize maswali mengi inavyo wezekana kuhusu hedhi na hali halisi kadri wanavyo endelea kukua.

BIBIY: Mwalimu katika kampeni hiyo tunataka pia kuzungumzia swala la kukosa kwenda shuleni wakati wa hedhi, wasichana wengi hasa katika maeneo ya vijijini hukosa kwenda shuleni kila mara wanapoanza siku zao za mwezi nafikiria kutokana na matatizo mbali mbali yanayowakabili.

TEACHER: Ni kweli kabisa unayosema Bibiy ... na sisi walimu tunafadhaishwa sana wakati wasichana wanapokosa kufika shuleni mara kwa mara na swala la siku za mwezi limekuwa ndio sababu kubwa kwa ..wasichana wengi kukosa kwenda shule wengine waohukosa kwenda shule kwa karibu siku tano kila mwezi kwa kuwa hawana vifaa maalum vya kujihifadhia wakati wa hedhi, ndiyo maana wengi wao wanaamua kubakia nyumbani kwa kuwa hawataki kupata aibu..utaona kwamba mwishowe msichana anakosa kufika shuleni kwa kiwango cha

asilimia 15 hadi 25 hali ambayo inawarudisha nyuma kimasomo na hilo linatutia wasiwasi mkubwa sisi walimu.

BIBIY: Je mwalimu unafikiri tutafanikiwa katika hiyo kampeni yetu?

TEACHER: Ndio Bibiy mimi nina hakika tutafanikiwa kwa sababu kampeni hii ni muhimu sana isipokuwa tunahitaji kuwashirikisha watalaamu wa afya ambao watazungumzia kuhusu matatizo mbali mbali yanayo sababishwa na kutokuzingatia usafi na pia wasichana watapata kuuliza maswali mengi yanayowatatiza kuhusu afya.Rossie natumai unaandika yale yote tunayojadiliana.

ROSSIE: Ndio mwalimu yote nimeyaandika..kutoka siku ya kwanza Bibiy alipoleta pendekezo hili.

TEACHER: sasa wasichana baada ya majadiliano yetu ya leo naona kuwa tuko tayari kabisa kuwasilisha pendekezo la kampeni yetu mbele ya afisa wa utamaduni na maswala ya jamii wa mkoa. Kesho tukijaaliwa tutakwenda kumuona.Nina hakika atapendezwa na kampeni yetu hii inayolenga kuwahamasisha wasichana juu ya usafi binafsi na maswala ya afya yanayohusiana na hedhi.

MUSIC............

SCENE TWO:
(Mwalimu na wanafunzi wake wako kwenye ofisi ya utamaduni ya mkoa)

OFFICER: Naam ninafuraha kupokea pendekezo lenu na ningependa kuwaambia kuwa kampenii hii iwapo itatekelezwa basi itawasaidia sana wasichana ili wapate kuendelea kubakia shuleni na pia watapata fursa ya kufahamu mengi juu ya afya yao, kwa hakika jamii nzima itanufaika, zamani swala la afya lilitumiwa tu wakati kampeni za kupambana na ueneaji wa maradhi zilipofanyika lakini siku hizi tunatumia ngazi hii pia

kueneza habari muhimu kuhusu usafi wetu binafsi na afya zetu kwa jumla lazima kila mtu ajiweke katika hali ambayo inakubalika na wengine.

TEACHER: Na sisi bwana afisa tumefurahi kuwa pendekezo letu limepokewa vyema,hakika wasichana wangu pamoja na mimi mwenyewe tutafurahi sana iwapo tutapata usaidizi wa hali na mali kwa hivyo nauliza vipi idara yako itakavyo tusaidia kufanikisha kampeni yetu hii?

OFFICER: kwa kweli hii ndio mara ya kwanza kwa idara yangu kupokea pendekezo la aina hii na jambo la muhimu ni kuwa pendekezo lenyewe limetolewa na wasichana kwa hivyo kwanza nataka kuwahakiishia kuwa ofisi hii itawajibika kwa kila njia kuona kwamba kampeni hii imefanikiwa kabisa..kwanza swala la usafiri msiwe na shaka idara yangu itafanya matayarishohii ni pamoja na fedha za malazi na chakula pia zitapatikana msiwe na shaka kabisa. Pia niwapa hongere sana kwa wazo hilo zuri.

BIBIY: Asante sana bwana afisa hata mimi pamoja na wenzangu tutajibidiisha kuifanikisha kampeni hiyo, ningependa pia kukujulisha kuwa katika kampeni hiyo tunatarajia kukariri mashairi na mchezo wa kuigiza mabali namazungumzo ya ana kwa ana na wasichana wenzetu tunapanga kuifanya kampeni yetu kabambe siku za wikiendi au wakati ambapo shule zitakuwa zimefungwa ili kuwavutia wasichana wengi.

OFFICER: Ooh!! Kwa kweli nyinyi ni kielelezo bora kwa jamii nataraji vijana wengine wataiga mfano wenu, maanake kuna maswala mengi yanayowahusu vijana ambayo yanahitaji kushughulikiwa ingekuwa vyema kwa vijana popote pale walipo kutafuta njia mbalimbali za kuwahamasisha vijana wenzao.

TEACHER: Ninajivunia sana wasichana wangu hawa wamefanya mambo mengi ya kupendeza na hasa hili la kutaka kuwahamasisha wasichana wenzao ili wazingatie afya na usafi ni swala ambalo kwa kweli sio rahisi kama linavyosikika likitajwa,

lakini nina hakika wasichana hawa watawajibika vilivyo hadi kampeni yetu ifanikiwe.

OFFICER: sawa kabisa mwalimu hata mimi sina shaka yoyote, na basi kwa sasa naona kila kitu kinakwenda sawa namimi nitahakikisha kuwa afisi yangu inawasiliana na wizara ya afya ili kuwaomba wawapatie watalaamu wa afya mtakao andamana nao. Kwa hivyo tutazidi kuwasiliana hadi hapo safari itakapowadia.
(Bibiy na wenzake wanafurahia).

MUSIC

ALMA: Lo! Bibiy umeleta pendekezo zuri sana unajua ni kweli kabisa kuwa wasichana wengi wanaona haya kuzungumzia swala la hedhi yaani huwa hawataki kabisa kutamka lolote juu ya siku za mwezi, wanaona ni sawa na kunywa dawa chungu.

BIBIY: Ni kweli Alma tena ujue wasichana wengi tu hawaelewi vyema namna ya kujihifadhi, halafu inakuwa ni aibu pale wavulana wanapokwambia eeh Fulani nguo yako imeharibika yaani mtu unajisikia vibaya kweli.(Anacheka) au wengine wanakutania wanakwambia eti .angalia umechora ramani ya Afrika (Wote wanacheka) Ndio maana wasichana wengi huwa wanaona ni afadhali wabakie nyumbani mpaka mtu amalize siku zake kuliko kupata aibu mbele ya wanafunzi wenzako.

ROSSIE: Yaani mimi nina isubiri kwa hamu siku hiyo tutakayoanza hiyo kampeni yetu, ninawaza vile tutakavyo simama mbele ya wasichana marika yetu kuwazungumzia. kwa kweli swala la usafi binafsi linatuhusu sisi sote hata tukifanyaje hatuwezi kuepuka hedhi..mimi nilipopata siku zangu kwa mara ya kwanza wala hata sikujua chochote maanake sikuwa nimeshaelezewa na mtu yoyote kuhusu siku za mwezi basi nikaa kimya hadi baada ya kama siku mbili hivi nilipoona mambo yanaendelea sikuweza kuvumilia tena ikanibidi nimwambie mama yangu.

BIBIY: Yeah!! Ndio maana ni muhimu kuendesha kampeni juu swala hili kwa kuwa kila msichana akijua yanayopasa kufanya basi sote tutakuwa hatuna hofu tena ya siku zetu na kila msichana atajua kuwa siku za mwezi ni jambo la kawaida maishani.

ALMA: Mimi hata sijui ni kwa nini wasichana wanaogopa wakati wakiingia kwenye siku zao..ninataka wakati huo tushirikiane na wenzetu ili tubadilishane mawazo na pia nitawahadithia kuhusu mimi mwenyewe. Niahakika tukibadilishana mawazo tutajifunza mengi.

BIBIY: Pia wenzangu tusisahau kuwakumbusha wazazi juu ya umuhimu wa kuwapa wasichana fedha za kununua taulo maalum na ambazo sio ghali kisha zinapatikana kwenye maduka mengi tu yaliyo karibu yetu isipokuwa jambo la muhimu ni kama vile mwalimu alivyotuambia kuwa tutilie mkazo swala la kuzingatia usafi wetu binafsi wakati wa siku hizo nyeti.

ROSSIE: kwa mfano ni muhimu kuoga japo mara moja kwa siku ukiwa katika hedhi kwa sababu unahitaji kuondoa harufu mbaya mwilini mwako, pili jaribu ikiwezekana kutumia taulo maalum kujihifadhi badala ya kitambaa.

ALMA: Jamani tusisahau pia kusisitiza umuhimu wa kuosha mikono baada ya kutoka msalani kujibadili ili kuepuka maambukizi..nafikiri ni muhimu pia kuwa tutaandamana na maafisa wa afya ili watupe mifano ya maambukizi ambayo tunaeza kupata kwa kutozingatia usafi hata sisi tutauliza maswali mengi tu.

BIBIY: Hey ...jambo linguine la muhimu ni.. usisahau kubadili nguo zako za ndani kila siku kwa kufanya hivyo una uhakika wa kuwa safi na fresh. (Wanacheka)

ROSSIE: Bibiy hiyo ni sawa kabisa maanake hata ukioga kila siku kisha usibadilishe nguo zako za ndani unakuwa ni kama umetoka kuogelea ndani ya tope..au ni sawa na kwenda

kucheza ndani ya jalala. Kwa hiyo ni muhimu sana kubadili nguo za ndani tena kila siku.

BIBIY: Na pia wenzangu sisi wasichana lazima tutambue kuwa ni muhimu kuwauliza wazazi wetu hasa mama zetu au wanawake watu wazima ambao tunawajua kuhusu mambo yanayohusiana na hedhi kwani bila shaka wao wanajua mengi na watatupa ushauri..tusione haya tujifunze kuukata ukimya na kuanza kuzungumza kwa uwazi kuhusu hedhi.

Autro: Na mpaka hapo ndio tumekamilisha sehemu ya nane ya mchezo kwa jina usafi na umuhimu wake ambapo Bibiy na wenzake wameamua kuanzisha kampeni ya kuwahamasisha wasichana wenzao juu swala hilo.Usikose kujiunga nasi kwenye sehemu ya tisa ya makala haya ya Jifunze Kwa Kusikiliza vilevile unaweza kuusikiliza tena mchezo huu au pia mwambie rafiki ausikilize kupitia kwenye tovuti yetu HYPERLINK "http://www.dw-world.de/lbe" www.dw-world.de/lbe  Hadi wiki ijayo kwaheri.